Maswali

1. Mungu alimchagua nani kuwa nabii?
2. Mungu alisema nini itafanyika wasipotubu?
3. Nani aliandika maneno yaliyonenwa na Yeremia?
4. Mfalme Yehoyakimu muovu alifanyaje hicho kitabu?
5. Yeremia na Baruku walifanya nini baada ya kitabu kuharibiwa?
6. Nini ilifanyika kwa mfalme Yehoyakimu?
7. Manabii na wakuu walifanyaje Yeremia alipowaletea ujumbe kutoka kwa Mungu?
8. Nani alimuokoa Yeremia?
9. Nini ilifanyika kwa mfalme Sedekia wakati Yerusalemu ilitekwa?
10. Nini ilifanyika kwa Yeremia? Nini ilifanyika kwa Ebedmeleki?

Majibu

1. Yeremia alichaguliwa kuwa nabii wa Mungu.
2. Wakaldayo wangekuja na kuharibu nchi yao.
3. Baruku aliandika maneno ya Mungu kwa kitabu.
4. Mfalme Yehoyakimu alikata kitabu kwa kisu na kukichoma.
5. Yeremia na Baruku waliandika maneno tena kwa kitabu kingine kwa siri.
6. Mfalme Yehoyakimu alichukuliwa mateka hadi Babeli.
7. Walimtupa Yeremia kwenye kisima cha matope.
8. Ebedmeleki aliokoa Yeremia. Alimvuruta kwa kamba.
9. Mfalme Sedekia alishikwa.Wanawe waliuwawa yeye alipofushwa na kupelekwa Babeli.
10. Yeremia alikubaliwa kukaa kwa nchi yake. Ebedmeleki aliokolewa.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2

29 Yeremia

Marejeo

Yeremia 36:1—8 na 19—23; Jeremia 38:1—13

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yeremia alimtii Mungu hata kuhatarisha maisha yake. Alijaribu kuokoa watu wake kutoka kwa Wakaldayo.Mungu hulinda wale wanaomtii.

Maneno maalum

1. Yeremia + nabii + hadharisha + tia moyo.
2. Watu wabaya + waovu + Wakaldayo + hadhari.
3. Yehoyakimu + waovu + Baruku + kitabu + moto + choma + kitabu kingine.
4. Nabukadreza + Sedekia + wafungwa + Babeli + Yeremia + ujumbe + sawa.
5. Ebedmeleki + matambara + okoa Yeremia.
6. Wakaldayo + kamata (shika) + wana wa Sedekia wauwawa + kuwa kipofu.
7. Yeremia alinda + Ebedmeleki.

29.1 Yeremia alipokuwa bado kijana, Mungu alimwambia kwamba alikuwa amemchagua kuwa nabii. Nabii ni mtu anayeonya watu na kuwatia moyo. Aliwambia watu maneno ya Mungu. Wakati mwingine nabii husema mambo yajayo.

29.2 Wakati wa utawala wa mfalme Yosia aliyekuwa mzuri, Yeremia alisaidia na kuwapa watu moyo. Baada ya kifo cha Yosia, wafalme waliofuata walikuwa waovu sana. Watu walimuacha Mungu tena. Kazi ya Yeremia ilitatizika kwa sababu watu hawakutaka kusikia maneno ya Mungu. Walimcheka na hawakuwa wazuri kwake, Yeremia aliwambia kwamba wanatakiwa watubu na wasikilize ujumbe wa Mungu. Aliwambia kwamba wasipomtii Mungu Wakaldayo watawasumbua. Nchi yao itaaribiwa. Yeremia alihuzunika sana alipoona Wakaldayo wakijitayarisha kuwapiga lakini watu hawakusikiliza ujumbe wenye Yeremia alileta kutoka kwa Mungu.

29.3 Mfalme Yehoyakimu alikuwa mwana wa Yosia lakini alikuwa mfalme muovu sana. Mungu akamwambia Yeremia aandike hadhari zote alizokuwa awaambie hao watu. Akamwambia aandike uovu wote waliokuwa wametenda. Yeremia akachukuwa kitabu akasema maneno yote yaliyokuwa yamesemwa na Mungu. Baruku mwandishi akayaandika hayo maneno yote katika kitabu. Hicho kitabu kikapelekewa mfalme Yehoyakimu. Mfalme Yehoyakimu alikuwa amekaa anaota moto ndani ya chumba kilichotumiwa wakati wa baridi. Walisomea mfalme hichi kitabu. Mfalme Yehoyakimu aliudhika sana aliposikia maonyo hayo ya Mungu kwamba Wakaldayo watakuja na kuharibu nchi yao. Zaidi sana ni kwamba yote aliyoyafanya yalikuwa maovu. Mfalme alikata kila kipande kilichosomwa. Alikata hicho kitabu na kisu. Kila alipokata alitupa motoni. Kilichomwa hata kikawa jivu. Mfalme Yehohakimu aliharibu kitabu lakini hakuharibu maneno ya Mungu. Mungu alimwambia Yeremia na Baruku waandike hayo maneno tena. Wakaandika maneno yote kwa kitabu kingine.

29.4 Maneno ya Mungu kitabuni yalikuwa ya kweli. Miaka michache baadaye, mfalme Nebukadreza wa Babeli alishambulia Yuda. Alichukuwa Yehoyakimu mfalme muovu mateka mpaka Babeli na kumtawaza Sedekia awe mfalme wa Yuda.

Lakini Sedekia alikuwa chini ya amri ya Nebukadreza. Mungu alimpa Yeremia ujumbe. Huu ujumbe wa Mungu ulitaka Sedekia, makuhani na wakuu wote watii mfalme Nebukadreza. Wakimtii mfalme Nebukadreza watakaa kwa amani katika nchi yao. Lakini wasipomtii, watachukuliwa mateka mpaka kwa nchi ya Babeli. Mfalme Sedekia, makuhani na wakuu hawakumsikia Yeremia. Walikataa kusikia ujumbe wa Mungu. Mfalme Sedekia aliasi, kwa hivyo mfalme Nebukadreza alikuja na kuuzunguka mji wa Yerusalemu.

Mungu akampa Yeremia ujumbe wa mfalme Sedekia tena. Yeremia alipompa mfalme Sedekia huo ujumbe, makuhani na wakuu walikasirika sana. Walimtupa Yeremia ndani ya kisima. Maji ya kisima yalikuwa yamekwisha lakini kulikuwa na matope chini. Yeremia alitumbukia ndani ya matope. Hangeweza kujitoa nje. Yeremia aliachwa ndani ya kisima kusudi afe kwa njaa na kiu.

29.5 Kulikuwa na mtu mwaminifu Yerusalemu. Aliitwa Ebedmeleki. Ebedmeleki alienda kumsihi mfalme Sedekia amuokoe Yeremia. Mfalme Sedekia alimpa Ebedmeleki ruhusa ya kumtoa. Ebedmeleki alichukuwa watu thelathini wamsaidie. Walimteremshia Yeremia kamba. Tena wakateremsha matambara na nguo mzee. Yeremia alijifunga kamba na akaweka matambara kwa mikono ili kamba isimkate. Ebedmeleki na rafiki zake walimtoa Yeremia kutoka kwa matope Walimuokoa kutoka kwa kisima.

29.6 Walkaldayo waliuzunguka Yerusalemu kwa miezi kumi na nane. Wakaishambulia Yerusalemu. Jeshi la Babeli lilivunja ukuta kwa kutumia magogo na kuingia ndani ya Yerusalemu. Wakaiba, wakachoma na kuiharibu. Watu wengi waliuwawa. Watu wengi walichukuliwa mateka mpaka Babeli. Mfalme Sedekia alijaribu kutoroka usiku Yeye na familia yake walijaribu kukimbilia ndani ya bustani ya mfalme wakitumia lango lililokuwa katikati ya ukuta lakini Wakaldayo waliwapata. Wana wa mfalme Sedekia waliuwawa mbele yake. Mfalme Sedekia alipofushwa macho na kupelekwa Babeli kwa minyororo. Lazima alijuta akiwaza kwamba kama angeskiza ujumbe wa Mungu.

29.7 Mfalme Nebukadreza alikuwa amesikia habari juu ya nabii Yeremia. Alisikia kwamba Yeremia alikuwa amemwambia Sedekia awatii Wakaldayo. Mfalme Nebukadreza alipeana amri isiyoyakawaida kwamba Yeremia asiumizwe. Yeremia alikubaliwa kukaa kwa nchi yake. Ebedmeleki naye alipona kwa sababu aliokoa Yeremia.